**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 Certified**

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*


## TAARIFA KWA WAFANYABIASHARA WA BIDHAA ZA CHAKULA NA VIPODOZI

**Dar es Salaam,Novemba 14, 2023**

Kwa mujibu wa Sheria ya Viwango, Sura 130 na kanuni zake Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na majukumu mengine limepewa jukumu la kusimamia usalama na ubora wa bidhaa za chakula na vipodozi kwa lengo la kulinda afya ya jamii. Katika kutekeleza jukumu hili, Shirika hutoa huduma ya usajili wa maeneo ya biashara yanayohusika na chakula, vipodozi, majengo ya kuuzia, kuandalia au kusambazia bidhaa hizo.

Maeneo ya biashara yanayohitajika kusajiliwa ni pamoja na hoteli za kitalii na za kawaida, supermarkets, maduka ya jumla na rejareja ya vyakula na vipodozi, mashine za kuchakata nafaka na mazao mengine yasiyofungashwa, wauzaji na wasambazaji wa chakula kwenye mikusanyiko (caterers), vioski, baa, maghala ya vyakula na vipodozi, kantini, migahawa na magari yanayobeba vyakula na vipodozi.

Usajili huu ni wa lazima na maombi yafanyike kupitia tovuti ya TBS (**www.tbs.go.tz**) kupitia mfumo wa maombi mtandao **https://oas.tbs.go.tz** kabla ya tarehe **31.12.2023**.

TBS inapenda kuwatahadharisha wafanyabiashara wote kuwa atakayekutwa anauza, anahifadhi au kusambaza bidhaa za chakula na vipodozi bila kusajili jengo lake atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800 110 827.**

Imetolewa na:

**Gladness H. Kaseka**
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**